

PRESS RELEASE

(DSE:SWALA)

2nd Floor Oyster Plaza, Plot No.1196 | TEL +255 (0) 755 687 785
Oysterbay, Haile Selassie Road,
P.O. Box 105266, DSM, Tanzania

22 February 2018

MAJIBU YA SWALA KUHUSU TAARIFA YA HIVI KARIBUNI YA TPDC KWA VYOMBO VYA HABARI

Swala Oil & Gas (Tanzania) ("Swala" au "Kampuni") imepata taarifa ya hivi karibuni ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania ("TPDC") kwa vyombo vya habari kuhusu makubaliano kati ya Swala na Orca Exploration Group Inc ("Orca") ambayo yalipelekea Swala kuwa mwana hisa wa PAE PanAfrican Energy Corporation ("PAEM") ("Makubaliano").

Makubaliano hayo yalikamilika tarehe 29 Desemba 2017. Swala imefanya jitihada za kuandaa kikao na TPDC kwaajili ya kufafanua makubaliano hayo mara mbili kati ya tarehe 2 Januari 2018 na tarehe 2 Februari 2018. Swala haikupokea majibu yoyote katika mawasiliano iliyofanya na TPDC na inakataa madai ya TPDC kwamba haija taarifiwa kuhusu makubaliano hayo. Swala itakuwa tayari kubainisha makubaliano hayo moja kwa moja lakini haitatoa tamko lingine zaidi kwa umma kuhusiana na jambo hili.

Kwa sasa Swala inashirikiana na Mamlaka ya masoko ya mitaji na dhamana (CMSA), Mamlaka ya Mapato Tanzania na Tume ya ushindani (Fair Competition Commission - FCC) kubainisha makubaliano na kuendelea ku-shirikiana na wadau wote wenye nia kadri inavyoendelea na mpango wake wa kupeleka hati fungani ya \$50 milioni katika soko la hisa la Dar Es Salaam DSE. Hati fungani hizo tayari zimesha amsha ari kubwa kwa taasisi mbalimbali nchini Tanzania na sehemu zingine za (EAC - East African Community) na kuhamasisha makampuni mengine nayo pia kutafuta uwekezaji katika Tanzania na kuorodheshwa katika DSE. Maoni ya TPDC yana-weza kutengeneza hali ya wasiwasi miongoni mwa wawekezaji wa ndani, ambao Swala inashirikiana nao kila mara.

Makubaliano hayo yamekidhi matakwa ya sheria zote zinazohusika. Kwa kupitia makubaliano haya Swala imepanua umiliki wa ndani usio wa moja kwa moja katika sekta ya nishati kitaifa na kimataifa, jambo linaloipatia Tanzania fursa mbadala ya ushiriki wa Tanzania katika sekta ya mali asili. Uwekezaji wa kigeni katika Swala, ikiwemo uwekezaji kutoka sehemu zingine za EAC, unaonyesha ujasiri wa kimataifa katika Agenda ya serikali kuhusu mapinduzi ya viwanda, ambayo upatikanaji wa nishati ya uhakika ni jambo la msingi. Mfumo wa fedha wa Swala, umeandaliwa maalumi kuhamasisha ushiriki wa taasisi za kitanzania, ikiwemo hati fungani ya kwanza katika sekta ya mafuta kuwepo katika soko la Hisa la Afrika mashariki na fursa ya urejeshaji wa malipo ya fedha kupitia malipo ya riba kwa wenye hati fungani.

Bwana Abdullah Mwinyi (Mwenyekiti wa Swala) amesema: "Kupitia makubaliano haya Swala inataka kusaidia dira ya maendeleo ya serikali ya Tanzania kwa namna mbalimbali za kivumbuzi. Inaendana sana na falsafa yetu ya kuchangia katika maendeleo ya ndani na kukuza uchumi wa Tanzania".

Dr. David Metres Ridge (CEO wa Swala) amesema: "Swala inashirikiana na wadau wote wenye nia kuhakikisha kuwa makubaliano hayo yanaeleweka kwa wote na inafanyakazi kwa pamoja na wadau hao wakati ambapo hati fungani yetu ya pili ya Mezzanine, (*mezzanine bond*) inaendelezwa. Tunachukulia ujumbe wa TPDC kwa umma kuwa hauna msaada katika maendeleo ya uwekezaji wa ndani na ushiriki katika miradi ya kimataifa na katika juhudi zetu za kusaidia maendeleo ya dhamana za ndani na soko la usawa (*equity market*). Wakati tunaendelea kujaribu kufafanua makubaliano haya na TPDC hatutashiriki katika majadiliano zaidi katika vyombo vya habari kuhusu suala hili."

PRESS RELEASE

(DSE:SWALA)

2nd Floor Oyster Plaza, Plot No.1196 | TEL +255 (0) 755 687 785
Oysterbay, Haile Selassie Road,
P.O. Box 105266, DSM, Tanzania

Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana na:

Swala Oil & Gas (Tanzania) plc

Ms. Janeth Mapundi

Janeth.mapundi@swalaoilandgas.com

www.swalaoilandgas.com

Kuhusu Swala:

Swala ni kampuni ya kwanza ya Mafuta na Gesi kuorodheshwa katika Soko la Hisa la Afrika Mashariki (East Africa Stock Exchange) likiwa na umiliki wa ndani. Swala inamiliki mali katika mfumo wa world-class East African Rift System. Ardhi yenye ukubwa kamili wa kilometa za mraba 14,000km². Pamoja na riba ya 7.93% katika PAE PanAfrican Energy Corporation. Uvunduzi mpya umetanganzwa na washirika wa sekta hii katika idadi kadhaa ya leseni katika mwelekeo huu ambao inapanua mabilioni ya uwekezaji wenye mafanikio ya Abert Grabel, inayoendelezwa na Tullow Oil katika ukanda wa mashariki wa bonde la ufa. Swala ina program zenye ufanisi na maendeleo ya biashara kuendelea kukuza uwepo wake katika kanda za hydrocarbon za Afrika Mashariki na Duniani kote.